

KARIBU

Karibu kwenye tovuti ya Taasisi ya De Borda, iliyopo Kaskazini mwa Ireland, ambayo inalenga katika kuhamasisha matumizi ya taratibu shirikishi za upigaji kura kwenye masuala yote ambayo yanagusa maamuzi ya kijamii.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tumia vielelezo vilivyopo kwenye ukurasa huu upande wa kushoto au wasiliana nasi kwenye Makao Makuu ya Taasisi. Taarifa za jinsi ya kuwasiliana nasi zimeainishwa kwenye tovuti hii hapa chini.

MALENGO YA TAASISI

Taasisi ya De Borda inalenga katika kuhamasisha matumizi ya taratibu shirikishi za upigaji kura kwenye masuala yote ambayo yanagusa maamuzi ya kijamii.

Malengo haya yanahusisha taratibu za kufanya maamuzi, zikiwa kwa chaguzi za mikoa au kitaifa, kwa wawakilishi wanaochaguliwa kwenye halmashauri na bunge, au kwa wanachama wa makundi ya kijamii, bodi za mashirika, vyama vya ushirika na kadhalika. Muundo unaopendekezwa kuwa sahihi ni ule wa Hesabu za Borda (HB) au vinginevyo mfumo ulioboreshwa zaidi, yaani Hesabu za Borda Zilizoboreshwa (HBZ).

Masuala ya maamuzi ya kijamii pia yanahusisha uchaguzi. Kwa sasa mifumo mingi ya uchaguzi ni kinzani, inayowaweka walio wengi dhidi au walio wachache zaidi dhidi ya wengineo, au sehemu moja dhini ya nyingine (kama ilivyo kwenye mifumo iliyo na uwiano). Katika mfumo wa upigaji kura ili kutoa idhini, kama ilivyo kwenye Mfumo wa Quota wa Borda (MQB), wapiga kura wanaweza kuwa washirika. Mpiga kura anapiga kura kwa idadi ya watu kwa mujibu wa mapendekezo yake, baadaye, katika kuhesabu kura, mapendekezo yote ya kura zote zilizopigwa yanajumuishwa, ushindi wa mgombea mmoja wakati mwingi ukitegemea na maoni (mapendekezo) ya wapiga kura wengi, kama sivyoyote, wapiga kura wote.

Taratibu Shirikishi za Upigaji Kura

Taratibu hizi zinapatikana katika nyanja kuu tatu.

Upigaji Kura Ulioboreshwa wa Borda (au Maoni): Mfumo huu unaweza kutumika wakati ambapo uamuzi unatakiwa kufanyika au sera inatakiwa kutumika.

Mfumo wa Quota wa Borda: Huu ni mfumo wa uchaguzi kwa kuchagua wawakilishi, wakati ambapo, kwenye mfumo wa uwiano, idadi maalum ya watu huchaguliwa.

Kura ya Mgawanyo: Mfumo huu wa uchaguzi hutumika wakati idadi timilifu ya watu wanapotakiwa kuchaguliwa kwenye nafasi zenye idadi hiyo timilifu, katika vyeo ambavyo, pengine ni tofauti, kama ilivyo ambapo Mkutano Mkuu unapochagua viongozi watendaji au bunge linapochagua baraza la mawazidi.

Peter Emerson,
Taasisi ya De Borda,
Barabara ya Ballysillan, Na. 36,
Belfast BT14 7QQ,
Ireland ya Kaskazini
Tel: +44 (0)28 9071 1795
Fax: +44 (0)28 9071 1795

pemerson@deborda.org